# Namna ya kujifunza na mtoto wako asiye na uwezo wa kusikia mkiwa nyumbani.

Deaf Child Worldwide

**Kutokana kuwepo na janga la virusi vya Corona, shule zimefungwa ulimwenguni kote. Kama mtoto wako kiziwi amerudi nyumbani kutokana na kufungwa kwa shule au hawezi kushiriki mafunzo katika shule za karibu na nyumbani, jambo hili ni changamoto sana na kama mzazi utakuwa na wasiwasi kwamba wanakosa elimu. Lakini kama mzazi na familia kwa ujumla wanaweza kuwa na mchango mkubwa katika kuhakikisha mtoto wao anaendelea kujifunza na kupata elimu.**

**Kitendo cha kujifunza kinaweza kutokea wakati wowote, katika kazi na shughuli za kila siku, katika majadiliano ya pamoja wakati wa chakula, wakati wa michezo au mawasiliano ya kawaida ndani ya familia, wakati wa usafi, kufua nguo na kupika chakula.**

**Elimu inayotolewa mashuleni na majumbani ni vitu viwili tofauti lakini vyote ni vya muhimu. Usiwe na wasiwasi na ondoa shaka kujaribu kutengeneza mazingira ya shule ukiwa nyumbani. Fikiria kutengeneza mazingira ambayo mtoto ataweza kujifunza mwenyewe/kiasili. Kumuonyesha mtoto namna ya kunawa mikono ni jambo la muhimu kama tu ambavyo angejifunza kupitia kusoma kitabu. Ziko njia nyingi za kukuza na kumfundisha mtoto stadi za maisha;**

- Kuhesabu vitu na kuonyesha idadi kwa kutumia vidole.
- Muelezee viungo ulivyotumia na namna vinavyobadilika wakati wa kupika.
- Msadie mtoto kuchagua herufi katika majina yao.
- Kuwafundisha kutaja muda.
- Kumtajia mtoto wako majina ya miti, vilima, mito ya maji, matunda, mbogamboga, wanyama na ndege na kisha kujadili na kukubaliana alama za hivyo vitu. Au kuelezea, kushika, kuonja au kunusa vitu hivyo ili kuweza kujifunza rangi, maumbo, ladha, harufu na muundo.

Mtoto wako anaweza kujifunza pindi akiwasiliana au kucheza na wewe au pamoja na watu katika familia, au hata mkiwa mmeongozana katika shughuli zako za kila siku.

# Namna ya kujifunza na mtoto wako asiye na uwezo wa kusikia mkiwa nyumbani.


Deaf Child Worldwide

## Kuwasiliana

Mkiwa nyumbani na mtoto wako hakikisha anatumia ipasavyo kifaa cha kukuza usikivu (shime sikio) kama anacho au teknolojia yoyote.



Kuwa mvumilivu pindi unapoona mtoto wako anapata shida kukuelewa, badala yake tafuta njia nyingine ya kumuelewesha na si kurudia sentensi.



Si lazima ujue Lugha ya Alama ili uweze kuwasiliana na mtoto wako asiye na uwezo wa kusikia, unaweza kutumia ishara au kuonyesha vitu au kwa pamoja mnaweza kutunga alama au ishara.

Ukiwa unaongea na mtoto kiziwi, ongea kwa taratibu (sio haraka sana na si polepole sana), usipige kelele wala kumkaripia wakati ukiwa unatumia lugha ya alama au kutoa ishara. Kumbuka mtoto asiye na uwezo wa kusikia ili aelewe vizuri kile kinachosemwa wanahitaji kuangalia uso wako au midomo ukiwa unatamka maneo/kuongea.



Mueleze vizuri mtoto wako kile unachotegemea katika tabia na elimu yake lakini pia ni vizuri kujiandaa/kuwa mwepesi kubadilika pindi uonapo mabadiliko au kitu kigeni kwenye tabia au masomo yake.
Kila familia ina mbinu tofauti juu ya masuala yahusuyo kujifunza – hakuna mbinu nzuri wala mbaya. Wekeni sheria na taratibu mbalimbali lakini pia ni viruzi kuwa mwepesi kuzibadilisha pindi uonapo vitu/mipango haiendi sawa.



Muwezeshe mtoto wako aweze kujiamini kwa kumpa sifa na hongera pindi afanyapo jambo zuri badala ya kumkemea na kumpa adhabu pindi afanyapo jambo baya.
Kumbuka mtoto wako anaweza kufadhaika na kuwa na wasiwasi pindi aonapo mabadiliko ambayo hayaelewi.



## Utaratibu

Watoto wengi hufarahia pindi wanapokuwa na utaratibu wa kufanya shughuli zinazojirudia kila siku. Kwa kuwa na utaratibu huu utawafanya wajisikie salama pindi waonapo mambo mageni kwao katika kipindi shule zimefungwa. Kubalianeni kwa pamoja na toa ufafanuzi juu utaratibu huo na kisha andika au chora kwa maneno au picha.

# Namna ya kujifunza na mtoto wako asiye na uwezo wa kusikia mkiwa nyumbani.

Deaf Child Worldwide

## Kujifunza

Watoto wengi hujifunza vizuri pindi wanapoweza kutoa maoni, mawazo na kushirikiana na watu wengine.

Mshirikishe mtoto wako asiye na uwezo wa kusikia katika shughuli mbalimbali za kifamilia, ikiwemo majukumu madogo madogo ya nyumbani, ikiwemo ushiriki mzuri katika michezo.

Kama una vitabu na picha mbalimbali muonyeshe mtoto wako mkiwa mnapiga hadithi na kujifunza alama na ishara.

Tunga hadithi ya kumuelezea mtoto wako au mwambie historia ya familia yenu. Watoto wengi hupenda kufanya michezo ya kushindana – mfano, je ni vitu vingapi wameweza kukusanya nyumbani au kwenye maeneo ya nje na kuweza kuviweka kwenye boksi dogo au mfuko. Muulize mtoto wako akufafanulie nini wameona na kiko wapi. Muulize mtoto wako akufafanulie ni nini wameona na kilikuwa wapi.

## Tabia

Sote tunafahamu jinsi ilivyo muhimu kujali na kuangalia afya ya mwili ya watoto wetu lakini pia ni muhimu kuangalia afya ya akili. Watoto wengi huwa na wasiwasi namna wanavyoona matukio ya sasa na mabadiliko katika utaratibu wao wa kila siku.

Angalia kama mtoto wako anakuwa na msongo wa mawazo/mfadhaiko kutokana na mabadiliko ya utaratibu wa kila siku na watu wanaowazunguka – kama wewe una msongo wa mawazo ni rahisi kwa mtoto wako kufahamu lakini anaweza asielewe kile kinachoendelea.

- **Tabia zao zinaweza kubadilika**
- **Wanaweza wakalia sana**
- **Wanaweza kuacha kutaka kula au kucheza**
- **Wanaweza kuwa na huzuni sana**

**→ Kujifunza pamoja na mtoto wako asiye na uwezo wa kusikia ni jambo linaloweza kuwa la kuchangamsha na kufurahisha!**